Jarida la Kiswahili Sanifu

Wahusika Wanawake kama Nyenzo ya Uwezeshaji: Uainishaji na Majukumu Yao katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed Khamis

Ondiso, Jenipher Dinah ondisojenipher@gmail.com
Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya

IKISIRI

Makala hii inachunguza wahusika wanawake kama nyenzo kuu ambayo Said Ahmed Mohamed Khamis ametumia kuwasilisha maudhui ya uwezeshaji wanawake katika riwaya tano teule: *Asali Chungu* (Mohammed, 1977), *Utengano* (Mohammed,1980), *Tata za Asumini* (Mohammed,1990), *Nyuso za Mwanamke* (Mohammed, 2010) na *Kamwe si Mbali Tena* (Mohammed, 2014). Makala inabainisha idadi na mgawanyiko wa wahusika wa kike katika riwaya hizo, inawaainisha kimuundo kwa uainishaji wa Wamitila (2008) wa wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi, na inafafanua mchango wa kila kundi kwa mihimili mitatu ya uwezeshaji ya Kabeer (1999). Utafiti ulikuwa wa kifani na kimseto uliofanywa maktabani, ambapo data zilikusanywa kwa usomaji wa kina na unukuzi wa matini, zikachanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo pamoja na matumizi ya takwimu rahisi katika majedwali. Matokeo yanaonyesha kuwa riwaya teule zina wahusika wanawake sabini na tano na kwamba kuna mgawanyo bayana wa kazi za kimaudhui. Wahusika wakuu wamebeba safari ya uwezeshaji kama mchakato, wahusika wasaidizi wamebeba utetezi wa wanawake wengine, nao wahusika wajenzi wamewakilisha hali halisi ya jamii inayohalalisha uwezeshaji. Mhusika anayeshindwa na mfumo, kama Asumini katika *Tata za Asumini* (Mohammed, 1990), naye ametumika kama kauli ya kimada dhidi ya ukandamizaji. Makala inahitimisha kuwa wingi na mgawanyo wa wahusika hawa ni uwekezaji wa makusudi wa mwandishi katika sauti za kike.

KUHUSU MAKALA

Maneno Muhimu:
Uainishaji wa wahusika, Uwezeshaji wanawake, Wahusika wanawake

Historia ya Makala:
Tarehe ya Kutumwa:17 Agosti 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 12 Sept 2026
Tarehe ya Kukubalika:15 Sept 2026
Mtandaoni: 09 Oktoba 2026

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254716272433; *Barua Pepe; ondisojenipher@gmail.com*
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Ondiso, J. (2026). Wahusika Wanawake kama Nyenzo ya Uwezeshaji: Uanishaji na Majukumu yao katika Riwaya za Said Mohammed Khamis 3(2), 99-109
© 2026
Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

1.0 Utangulizi

Wahusika ndio uti wa mgongo wa kazi yoyote ya kifasihi. Wamitila (2003) anaeleza kwamba wahusika ni viumbe wa hadithi wanaopewa uhai na majukumu na mwandishi ili kufikisha ujumbe na kuakisi jamii. Naye Said Ahmed Mohamed mwenyewe, katika *Kunga za Nathari ya Kiswahili* (Mohamed, 1995), anaeleza kwamba mhusika ndiye chombo kikuu kinachotumiwa na msanii kuyapa maudhui yake mwili na sauti. Kwa hivyo, katika mjadala wa uwezeshaji wanawake katika fasihi ya Kiswahili, swali la msingi si maudhui gani yanawasilishwa pekee, bali pia ni nani anayeyabeba. Mwandishi amewaumba wahusika wa kike wangapi, wa aina gani, na wamepewa majukumu yapi? Majibu ya maswali haya ndiyo yanayoonyesha kama mwanamke ni pambo la pembeni au kiini cha simulizi.

Said Ahmed Mohamed Khamis ni mwandishi ambaye ameandika riwaya kumi na tano kwa kipindi cha zaidi ya miongo mitatu, na katika kipindi hicho chote amekuwa akiusaili msimamo wake kuhusu wanawake katika jamii. Riwaya zake tano zilizoteuliwa kwa makala hii zinasheheni wahusika wa kike sabini na tano, ambao wamegawanyika hivi: *Asali Chungu* 14, *Utengano* 14, *Tata za Asumini* 14, *Nyuso za Mwanamke* 17 na *Kamwe si Mbali Tena* 16. Huu ni uwanja tajiri wa kuchunguza matumizi ya wahusika wa kike kama nyenzo ya kimaudhui. Kichocheo cha makala hii kinatokana na shauku ya kiusomi iliyomchochea mtafiti baada ya kusoma tafiti za Fakih (2017), Mugambi (1983), Osoro (2003), Ruto (2015) na Suakei (2013) kuhusu riwaya za Khamis, pamoja na antholojia ya Bertoncini-Zúbková (1996) iliyoziweka riwaya zake za mwanzo kwenye ramani ya usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Tafiti hizi zimewaangazia wahusika wa kike katika riwaya za Khamis kwa mtazamo wa taswira na matatizo yao, nazo zimeacha nafasi ya uchunguzi wa kimfumo wa muundo wa wahusika hao, yaani idadi yao katika riwaya zote tano, uainishaji wao kwa vigezo vya nadharia ya uhusika, na mgawanyo wa majukumu yao katika kuwasilisha maudhui ya uwezeshaji. Makala hii inanuia kujaza nafasi hiyo.

Kwa hivyo, makala hii ilichunguza madhumuni matatu, yaani kubainisha idadi na mgawanyiko wa wahusika wanawake katika riwaya teule, kuwaainisha kimuundo, na kufafanua mchango wa kila kundi kwa maudhui ya uwezeshaji wanawake.

2. Uhakiki wa Maandishi

2.1. Dhana ya Wahusika na Uainishaji Wao

Nadharia ya uhusika imejengwa na wataalamu wa vipindi mbalimbali, kuanzia wa mwanzo hadi wa hivi karibuni. Forster (1927) alitofautisha wahusika bapa, wanaojengwa kwa wazo au sifa moja na wasiobadilika, na wahusika duara, walio tata na wenye uwezo wa kumshangaza msomaji kwa njia ya kuaminika. Kwake, mhusika mkuu kwa kawaida ni duara kwa sababu mabadiliko yake ndiyo huunda maana ya hadithi. Frye (1957) alisisitiza kwamba mhusika mkuu anayevutia huwa na lengo mahususi analolipigania na uwezo wa kubadilika kadri usimulizi unavyoendelea. Harvey (1965) alipanua mtazamo huu kwa kubainisha ngazi tatu za wahusika, yaani wahusika wakuu, wahusika wa mandhari ya nyuma wanaounda ulimwengu wa hadithi, na wahusika wa kati wanaotumia msuko na safari ya mhusika mkuu. Chatman (1978) aliuona uhusika kama mkusanyiko wa sifa zinazojengwa katika usimulizi, naye Phelan (1996) alionyesha kwamba mhusika hufanya kazi kwa njia tatu kwa wakati mmoja, yaani kama picha ya mtu halisi, kama chombo cha maudhui, na kama sehemu ya ufundi wa simulizi. Misingi hii ya awali imeendelea kutumika na kuendelezwa katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili wa hivi karibuni, kama inavyodhihirika katika kazi za Muia na wenzake (2023), Wafula na Njogu (2007) na Wamitila (2008).

Kwa upande wa uandishi bunifu, Card (1988) alieleza kwamba wahusika hupangwa kwa umuhimu wao, na kwamba wanaomzunguka mhusika mkuu ndio hujenga jamii ambamo anaishi na kutenda.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba mhusika mkuu huhusishwa katika kazi nzima, tangu mwanzo hadi mwisho, ukuu wake ukitokana na kubeba maudhui makuu ya mwandishi. Wahusika wasaidizi humzingira mhusika mkuu na kumpa msukumo wa kufanya uamuzi, nao wahusika wajenzi hutambulika kwa wingi wao na hujenga mazingira ambamo mhusika mkuu huishi. Uainishaji huu, ambao Wamitila (2002) anauweka kuwa mojawapo ya misingi ya uhakiki wa fasihi na ambao Mohamed (1995) mwenyewe anauelezea kwa mtazamo wa mwandishi, hupata maana yake kamili unapofungamanishwa na nadharia inayoeleza maudhui yanayobebwa na wahusika (Wafula & Njogu, 2007). Kutokana na fasili hizi, ni bayana kuwa mhusika si jina tu la mtu wa hadithi bali ni nafasi ya kimuundo yenye kazi ya kimaudhui. Katika makala hii wahusika wa kike wa Khamis wamechunguzwa kama nafasi za kimuundo, yaani

wakuu, wasaidizi na wajenzi, na kila nafasi imepimwa kwa maudhui ya uwezeshaji inayoyabeba.

2.2. Dhana ya Uwezeshaji Wanawake

Dhana ya uwezeshaji wanawake ilipata uzito mkubwa katika mijadala ya maendeleo kuanzia miaka ya 1980, ikichochewa na harakati za wanawake zilizopinga mfumo wa ubabe-dume na miundo ya tabaka, rangi na dini (Kabeer, 1999), na ikapata sura ya kimataifa katika Azimio la Beijing (United Nations, 1995). Keller na Mbewe (1991) wanaieleza kama mchakato ambao kwao wanawake hujipanga ili kuongeza uwezo wao wa kujitegemea, kudai haki zao, kufanya uchaguzi na kudhibiti raslimali. Sen (1993) anasisitiza kuwa uwezeshaji hubadilisha mahusiano ya mamlaka yanayobana uchaguzi wa wanawake; Batliwala (1994) anauona kama mchakato wa kisiasa unaohitaji hatua za pamoja; nao Schuler na Hashemi (1994) wanauona kama mchakato endelevu wa kufikia fursa za uchumi, elimu na afya. Rowlands (1995, 1997, 1998) alibainisha kwamba uwezeshaji hujitokeza katika nyanja ya mtu binafsi, ya mahusiano ya karibu na ya pamoja, na kwamba huhusisha jinsia zote. Kabeer (1999) aliufafanua kama upanuzi wa uhuru wa mtu kufanya uchaguzi wa kimkakati wa maisha katika muktadha ambapo uhuru huo haukuwepo hapo awali, na baadaye akatofautisha upatikanaji wa raslimali na udhibiti wake (Kabeer, 2005). Wataalamu wa upimaji, kama vile Malhotra na wenzake (2002) na Mosedale (2005), wanakubaliana kuwa uwezeshaji ni mchakato unaopaswa kupimwa kwa viashiria mahususi, naye Cornwall (2016) anaonyesha kwamba kinachofanya kazi ni kujipanga kwa wanawake wenyewe kutoka chini. Kutokana na fasili hizi, katika makala hii dhana ya uwezeshaji wanawake imefasiriwa kama mchakato unaopimika kwa mihimili mitatu ya Kabeer (1999), yaani raslimali, uamuzi na mafanikio, unaobebwa na wahusika wa kike wa riwaya teule. Kando na mijadala ya kimaendeleo, dhana hii imechunguzwa pia katika fasihi ya Kiswahili, ambapo Msokile (1993) anaonyesha usawiri wa mwanamke kama mkombozi katika riwaya, Bertoncini-Zúbková (1996) anafuatilia usawiri wake katika nathari ya karne ya ishirini, naye Gromov (2022) anauchunguza katika nathari ya waandishi wa kike wa karne hii.

2.3. Wahusika Wanawake katika Riwaya ya Kiswahili

Uchunguzi wa kina zaidi wa usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili ni antholojia ya Bertoncini-Zúbková (1996), ambayo, kama kichwa chake *Vamps and Victims* kinavyodokeza, ilibaini kwamba mwanamke wa nathari ya Kiswahili ya karne ya ishirini alisawiriwa mara nyingi kwenye ncha mbili, ya mhanga au ya mrembo-hatari; iliziweka *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1980) na *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990) chini ya kichwa cha utoto na ujana, na *Utengano* (Mohamed, 1980) chini ya ndoa na umama, kabla ya kufunga na sehemu ya wanawake wa kisasa. Bertoncini-Zúbková na wenzake (2009) wanaziweka riwaya za Mohamed kwenye mstari wa mbele wa riwaya hiyo ya kisasa.

Rosa katika *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1980) ndiye kielelezo cha kizazi cha mwanamke-mhanga cha miaka ya 1970: anajaribu kujikwamua kutoka mazingira duni lakini anakumbana na vikwazo vinavyompelekea kuangamia; Muia na wenzake (2023), wakilinganisha wahusika wakuu wa *Rosa Mistika* na *Maisha Kitendawili*, wanatambua mchango wa Kezilahabi na Habwe katika kuwakilisha matatizo ya wanawake. Katika riwaya ya *Kuli* (Shafi, 1979), mwanamke amechorwa kama mkombozi katika uwanja wa kisiasa, kiuchumi na kifikra (Msokile, 1993). Kuanzia miaka ya 1990, waandishi wa kike wamekuwa mstari wa mbele katika kuwapa wanawake nafasi ya mhusika mkuu anayebadilisha hali yake; Gromov (2022) anaonyesha kwamba nathari ya waandishi wa kike wa Kiswahili wa Kenya wa karne ya ishirini na moja, akiwemo Clara Momanyi katika *Tumaini* (Momanyi, 2006) na *Nakuruto* (Momanyi, 2009), inaendelea kuyasawiri matatizo ya kizazi kipya, hasa ya msichana anayekataa kuozwa mapema na kudai elimu. Hata hivyo, Osoro (2003), akihakiki riwaya nne za Khamis kwa misingi ya kifeministi, alitahadharisha kwamba ingawa kuna maendeleo, bado kuna mitindo ya kuwafunga wanawake katika nafasi za kimapokeo. Mapitio haya yanaonyesha kwamba usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Kiswahili umejadiliwa hasa kama maudhui; makala hii inauliza swali la kimuundo: wahusika wa kike wamepangwa vipi, na mpangilio huo unabeba maudhui gani?

2.4. Tafiti za Awali kuhusu Wahusika wa Kike katika Riwaya za Khamis

Utafiti uliozaa makala hii umebaini kuwa tafiti zilizohakiki riwaya za Khamis kwa mtazamo wa mwanamke ni pamoja na Fakih (2017), Mugambi (1983), Osoro (2003), Ruto (2015) na Suakei (2013). Utafiti wa Mugambi (1983) unachunguza kilio cha wanyonge katika riwaya za mwanzo za Said Ahmed Mohamed, ukionyesha jinsi wanyonge, wakiwemo wanawake, wanavyodhalilishwa katika mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Utafiti huu

ni afiki katika makala hii kwa sababu unaweka bayana hali ya ukandamizaji ambayo dhidi yake uwezeshaji hupimwa. Hata hivyo, utafiti wa Mugambi (keshatajwa) unatofautiana na makala hii kwa sababu ulijikita katika uhanga wa wanyonge kwa jumla, si katika muundo wa wahusika wa kike wala mchango wao kwa uwezeshaji.

Utafiti wa Osoro (2003) unahakiki riwaya nne za Khamis, yaani *Asali Chungu*, *Utengano*, *Kiza katika Nuru* na *Tata za Asumini*, katika misingi ya kifeministi, ukitenga sura moja kwa usawiri wa wahusika wa kike. Utafiti huu ndio wa karibu zaidi na makala hii kwa sababu unawashughulikia wahusika wa kike moja kwa moja. Hata hivyo, utafiti wa Osoro (keshatajwa) unatofautiana na makala hii kwa sababu uliegemea nadharia ya ufeministi, ulishughulikia riwaya za mwanzo pekee, na haukuwahesabu wala kuwaainisha wahusika hao kwa vigezo vya nadharia ya uhusika.

Utafiti wa Suakei (2013) unachunguza usasa na mwanamke wa kisasa katika *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010) kwa nadharia ya ufeministi, ukionyesha changamoto zinazomkabili mwanamke wa kisasa na jinsi Nana anavyofaulu kupambana nazo. Utafiti wa Ruto (2015) unalinganisha matatizo yanayomkabili mwanamke katika *Kidagaa Kimemwozea* na *Nyuso za Mwanamke*, ukibainisha aina za unyanyasaji na jinsi wanawake wanavyojiepusha nazo. Naye Fakih (2017) alilinganisha usawiri wa mwanamke katika *Utengano* (Mohamed, 1980) na *Kamwe si Mbali Tena* (Mohamed, 2014) kwa nadharia ya fasihi linganishi na kubaini mabadiliko kati ya riwaya hizo mbili. Tafiti hizi tatu ni afiki katika makala hii kwa sababu zinapambanua riwaya za kisasa za Khamis, zenye idadi kubwa zaidi ya wahusika wa kike. Hata hivyo, zinatofautiana na makala hii kwa sababu kila moja ilishughulikia riwaya moja au mbili, na hakuna iliyoupima muundo wa wahusika wa kike katika riwaya tano kwa kipimo kimoja.

Kwa muhtasari, udurusu wa tafiti za awali umebainisha kuwa wahusika wa kike katika riwaya za Khamis wamejadiliwa hasa kwa mtazamo wa taswira na matatizo yao, na mara chache kwa mtazamo wa muundo wao na mgawanyo wa majukumu yao ya kimaudhui. Pili, umeonyesha kuwa hakuna utafiti uliowahesabu, kuwaainisha na kuupima mchango wa kila kundi kwa uwezeshaji katika riwaya zote tano. Hivyo basi, makala hii inaziba mwanya huo.

3. Mbinu za Utafiti

Makala hii inatokana na utafiti wa kifani na kimseto uliofanywa maktabani katika taaluma ya fasihi andishi, utanzu wa riwaya. Idadi lengwa ilikuwa riwaya kumi na tano za Khamis, na kutoka kwazo riwaya tano ziliteuliwa kwa usampulishaji wa kimaksudi (Bryman, 2004) kwa vigezo vya wingi wa wahusika wa kike, uzito wa maudhui ya uwezeshaji na mtawanyiko wa vipindi vya uchapishaji, nazo ni *Asali Chungu* (Mohamed, 1977), *Utengano* (Mohamed, 1980), *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990), *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010) na *Kamwe si Mbali Tena* (Mohamed, 2014). Data zilikusanywa kwa usomaji wa kina na unukuzi wa matini (Kothari, 2004), ambapo kila mhusika wa kike alitambuliwa, alihesabiwa na kuainishwa kwa mihimili minne ya Wamitila (2008), nayo matendo, maamuzi na kauli zake zilinukuliwa kwa kurasa na kusimbwa kwa mihimili mitatu ya Kabeer (1999). Uchanganuzi ulifuata hatua tatu za Bogdan na Biklen (1992), yaani uhariri, usimbaji na ufafanuzi wa kina, nayo matokeo yamewasilishwa kwa maelezo na kwa takwimu rahisi katika majedwali. Utafiti ulizingatia maadili ya kitaaluma na ulipata kibali cha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro na cha NACOSTI.

4.0 Matokeo ya Utafiti na Mjadala

Matokeo yanawasilishwa kwa mujibu wa madhumuni matatu ya makala. Sehemu ya 4.1 inabainisha idadi na mgawanyiko wa wahusika wanawake, sehemu ya 4.2 inawaainisha kimuundo, nayo sehemu ya 4.3 inafafanua mchango wa kila kundi kwa maudhui ya uwezeshaji.

4.1. Idadi na Mgawanyiko wa Wahusika Wanawake

Utafiti ulibaini jumla ya wahusika wanawake sabini na tano katika riwaya tano teule, wastani wa kumi na tano kwa riwaya. Jedwali la 1 linaonyesha mgawanyiko wao na hadhi wakilishi za wahusika hao.

Jedwali katika Tak.1 linaloonyesha idadi na hadhi wakilishi za wahusika wanawake katika riwaya teule, mambo matatu yanajitokeza; Kwanza, uwekezaji wa Khamis katika sauti za kike ni wa mfululizo; hakuna riwaya yenye wahusika wa kike chini ya kumi na wanne, tangu kazi ya 1977 hadi ya 2014, jambo linaloonyesha kwamba ajenda ya mwanamke si nyongeza ya baadaye katika uandishi wake bali ni nguzo yake ya kudumu.

Riwaya	Mwaka	Wahusika wanawake	Wahusika wanawake na hadhi wakilishi
Asali Chungu	1977	14	Mama na msichana wa kawaida (Bi. Pili, Semeni); mke wa tabaka la juu (Bi. Amina); wanawake wa mikutano ya hadhara (hawakupewa majina)
Utengano	1980	14	Mfanyakazi wa kasri (Biti Kocho); mke na binti wa kasri (Bi. Tamima, Maimuna); mwokaji mikate (Bi. Farashuu); mwenye klabu (Biti Sururu); mzungumzaji wa jukwaani (Kazija)
Tata za Asumini	1990	14	Wanafunzi wa chuo (Asumini, Miriam, Mwomboje); kiongozi wa umoja wa kina-mama (Miriam); mjasiriamali (Da Rupia)
Nyuso za Mwanamke	2010	17	Mwanafunzi, mwimbaji, mjasiriamali na Mkurugenzi Mkuu (Nana); mama mwenye akiba benki (Bi. Mkubwa); mke anayedai talaka (Shemsa)
Kamwe si Mbali Tena	2014	16	Mkulima na mdai-haki mahakamani (Bi. Chani); profesa (Samira); kiongozi wa vuguvugu (Mwavile); mke anayedai talaka (Jokha)
Jumla	1977–2014	75	Kutoka vijakazi na wake tegemezi hadi profesa, mkurugenzi mkuu na viongozi wa harakati

Tak.1: Jedwali la Idadi na Hadhi Wakilishi za Wahusika Wanawake katika Riwaya Teule

Pili, idadi inaongezeka katika riwaya za kisasa, yaani *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010) na *Kamwe si Mbali Tena* (Mohamed, 2014), na ongezeko hilo linaambatana na kupanda kwa hadhi, kutoka vijakazi na wake wa kasri wa riwaya za mwanzo hadi profesa, mkurugenzi mkuu na kiongozi wa vuguvugu wa riwaya za baadaye. Tatu, wingi huu unazaa sauti-nyingi; Khamis haandiki hadithi ya mwanamke mmoja bali ya jamii ya wanawake, ambamo mjakazi na mke wa kasri, mwokaji mikate, mwanafunzi wa chuo na profesa wote wanapata nafasi ya kusikika. Kimsingi, matokeo haya yanaonyesha kuwa idadi na hadhi za wahusika wanawake ndizo zinazomwezesha mwandishi kuonyesha uwezeshaji si kama tukio la kipekee bali kama mchakato unaowagusa wanawake wa tabaka, rika na mazingira mbalimbali, kama Kabeer (1999) anavyosisitiza.

4.2. Uainishaji wa Wahusika Wanawake Kimuundo

4.2.1. Wahusika Wakuu: Wabebaji wa Safari ya Uwezeshaji

Kila riwaya teule inaongozwa na mhusika mkuu wa kike anayebeba mchakato mzima wa uwezeshaji, kwa mtindo wa mhusika duara wa Forster (1927). Wahusika hawa wanajadiliwa kwa mpangilio wa mwaka wa uchapishaji ili kuonyesha mwelekeo wa usawiri wao. Semeni katika *Asali Chungu* (Mohamed, 1977) anaonyesha lengo mahususi la Frye (1957) kwa njia ya kimaadili, akikataa ombi la Bwana Zuberi kwa maneno haya, “Kweli sina haki ya kukataa matakwa yako, lakini... jambo ulitakalo ni zito kwangu” (uk. 17), akithamini heshima yake kuliko pesa.

Maimuna katika *Utengano* (Mohamed, 1980) anawakilisha kizazi kipya kilicho katika mtafaruku wa mila na mabadiliko. Mtunzi anaeleza kuwa kutoka nje kwake ni nadra, amenyimwa uhuru wa kutoka na amemtii babake siku zote bila swali (uk. 22–23). Kisha moyo unamzaini ajinyakulie uhuru wake kwa nguvu, na anaamua kuvunja minyororo ya utumwa wa kimila kwa kutoroka (uk. 23), akitaka:

> *azaliwe upya, aishi upya, alelewe upya asomeshwe upya, aishi katika ulimwengu aliokuwa akinyimwa kuishi. (uk. 23)*

Hata baada ya kutoroka, katika mazingira hatari kama danguro la Mama Jeni, anaonyesha uwezo wa kujilinda anapomkataa James kwa neno moja thabiti, “Sitaki”, na kujikwapua kutoka mikononi mwake (uk. 56). Katika mhimili wa uamuzi wa Kabeer (1999), anafafanua lengo lake mwenyewe na kulifanyia kazi hata bila raslimali za kutosha.

Asumini katika *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990) ni mhusika mkuu wa aina ya pekee. Vitabu alivyobugia vinampa nguvu na uhai mpya na uwezo wa kudadisi ukweli na uongo (uk. 5), lakini mfumo kandamizi wa familia na jamii unamshinda hadi

kifo. Katika barua yake ya mwisho kwa Sewa mtunzi anamnukuu akiandika:

> *Tafadhali nisamehe-ulimwengu umenishinda...Ole wake hii nafsi yangu iliyolemazwa na kuharibiwa: nisamehe; sikuweza kudumu kileleni tulikofikia... nimedhulumiwa na mama, nimedhulumiwa na mazingira yaliyonizunguka tokea utoto. (uk. 170-171)*

Kifo chake si udhaifu wa mhusika bali ni kauli ya kimada ya mwandishi. Bila raslimali na uhuru wa uamuzi, mzinduko wa ndani pekee hautoshi, kama Kabeer (2005) anavyotofautisha upatikanaji wa raslimali na udhibiti wake.

Nana katika *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010) anaanzia kwenye uasi wa ujanani. Mtunzi anamnukuu akisema, "Nilitaka kwa mara ya mwanzo n'ende kinyume na babangu bila kujali kungetokea nini" (uk. 34). Anakataa kupelekwa shule na kurudishwa kwa gari la madereva wa babake (uk. 38), anakataa mchumba aliyechaguliwa na babake (uk. 44), na anatamka falsafa yake ya kujitegemea kwa maneno yasiyoacha shaka:

> *Sikukuzwa kibarubaru ili niwe mwanamke wa kudanganyia. Nilizaliwa mwanamke nikakuzwa mwanamke – tena mbali na mamangu. Kwa hivyo nilihisi lazima nipigane mwenyewe kuwa mwanamume katika macho ya watu wanaoniona mwanamke. (uk. 108)*

Safari yake inafikia kilele cha kujenga ghorofa ya "Karibu Mwanamke" yenye vitengo vya huduma kwa wanawake na bendi ya taarab inayozalisha ajira (uk. 187–198), akiwa Mkurugenzi Mkuu ambaye babake Faisal anahudumu chini yake kama msaidizi-mshauri (uk. 196). Hapa mihimili yote mitatu ya Kabeer inakamilika.

Samira katika *Kamwe si Mbali Tena* (Mohamed, 2014) anafikia uprofesa wa Media na Information Technology katika chuo kikuu kimoja cha Sydney (uk. 200), na vuguvugu la mabadiliko linapopamba moto Zahran na Tambo wanamwomba arudi nyumbani kusaidia shughuli za itikadi na uenezi (uk. 200–201). Mafanikio ya mtu binafsi yanageuzwa kuwa raslimali ya umma, kwa mujibu wa nyanja ya pamoja ya Rowlands (1995, 1998).

Kimsingi, matokeo haya yanaonyesha kuwa wahusika wakuu wa Khamis wanatimiza kigezo cha Wamitila (2008) cha kuhusishwa katika kazi nzima, na ndio wanaobeba safari yenyewe ya uwezeshaji kama mchakato. Kati ya kuaga kwa Asumini aliyeshindwa na kurejea kwa Samira mshindi, mwandishi anachora upeo mzima wa hatima za mwanamke.

4.2.2. Wahusika Wasaidizi: Watetezi na Wawezeshaji wa Wenzao

Kundi la pili linabeba jukumu tofauti, yaani uwezeshaji wa wanawake wengine. Bi. Pili katika *Asali Chungu* (Mohamed, 1977) anamkabili DC Zuberi kwa shauri la Semeni (uk. 5–6), akiongoza wanawake wenzake katika kutetea haki zao. Katika *Utengano* (Mohamed, 1980), Biti Kocho, mfanyakazi wa kasri, anamzuia Maksuudi kumpiga Bi. Tamima na kumshauri akubali talaka (uk. 52–53), naye mtunzi anamnukuu akimwambia dhalimu huyo waziwazi:

> *Mabwana zaidi kuliko wewe sisi tuliwaondoa na penye haki sioni uzito wa kukuita jina lolote. Na ujue kuwa, wakati utafika wanawake kuonekana watu. (uk. 53)*

Kazija naye anavuka mpaka wa nyumbani hadi jukwaani, akifichua maovu ya Maksuudi kwenye mkutano wa kampeni za ubunge na kuwauliza wananchi, "Huyu Maksuudi ambaye ameshindwa kuiendesha nyumba yake ataweza kuangalia maslahi yetu?" (uk. 80–81), akiwachochea kumwondoa madarakani. Katika *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990), Miriam, mkuu wa Umoja wa Kina-mama wa taifa zima mwenye dhamana serikalini (uk. 112), anamzindua Asumini kwa kauli, "Mwanamke ni yule anayejua anataka nini" (uk. 51), naye Mwomboje anamweleza kwamba imani si kujigubika bali ni matendo (uk. 51). Katika *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010), Bi. Mkubwa anamwezesha bintiye kwa raslimali, akimwandikia:

> *Nimehakikisha kwamba nikutengenezee msingi wa kujitegemea kwa maisha yako ya baadaye, kwani mwanamke hawezi kuwa huru kama hana msingi wa kujitegemea kiuchumi. (uk. 172)*

Naye Shemsa, katika kipindi cha "Dukuduku" cha televisheni ya Nana, anasimulia jinsi alivyodai talaka, "ilinibidi nidai talaka, hata wazee wangu wangeniachia radhi namna gani" (uk. 211). Katika *Kamwe si Mbali Tena* (Mohamed, 2014), Bi. Chani, akiwa msichana, anawalazimisha wazazi wake wampeleke shule wakati watoto wa kike

hawakupelekwa (uk. 94–95). Ukubwani analiendesha shamba lake la matunda kukimu familia ya watoto tisa (uk. 195), na anapigania kesi ya ardhi hadi mahakamani, ambako kauli yake, “Sheria za ukoloni mnazoziendeleza zibadilisheni. Sheria za ruhusa zisiwepo tena tunapodai haki zetu” (uk. 212), inafuatwa siku hiyohiyo na uamuzi wa mahakama wa kurejesha mashamba kwa wananchi (uk. 213). Jokha naye anakataa mateso ya ndoa yake na kudai talaka (uk. 185–186).

Wahusika hawa wanadhihirisha kwamba, kwa Khamis, uamuzi wa mwanamke mmoja mara nyingi huwa raslimali ya mwanamke mwingine. Barua ya Bi. Mkubwa ni urithi wa Nana, nao utetezi wa Biti Kocho ni ukombozi wa Bi. Tamima. Hii ndiyo nyanja ya pamoja ya Rowlands (1995, 1998), na hapa ndipo mbegu za hatua za pamoja za Batliwala (1994) zinapopandwa. Kundi hili pia linabeba utata wa kimaadili. Bi. Farashuu katika *Utengano* (Mohamed, 1980) ni mchumi hodari, “mchumi kwelikweli. Yeye kazi tu, hataki mchezo” (uk. 28), lakini pia ni mwendeshaji wa kisasi dhidi ya Maksuudi kinachomwathiri Maimuna (uk. 32), naye Bi. Amina katika *Asali Chungu* (Mohamed, 1977) anatoa hundi kumhonga Dude ili avunje uhusiano wake na bintiye (uk. 162). Kimsingi, matokeo haya yanaonyesha kuwa wasaidizi wa Khamis ndio daraja kati ya uwezeshaji wa kibinafsi wa wakuu na mabadiliko ya jamii nzima, na kwamba kuwapa maslahi na makosa yao kunaifanya hoja ya uwezeshaji kuwa ya kuaminika badala ya kuwa mahubiri.

4.2.3. Wahusika Wajenzi: Sauti ya Umma na Hali Halisi ya Jamii

Kundi la tatu, ingawa halina kina cha kibinafsi, hubeba jukumu la kimuundo lisiloweza kuachwa, yaani kuwakilisha hali halisi ya jamii. Wanawake wa mikutano ya hadhara katika *Asali Chungu* (Mohamed, 1977), ambao hawakupewa majina, wanatoa hamasa ya pamoja kwa kauli, “Ikiwa hatuwezi kwa vitendo, japo kwa maneno tutasema” (uk. 13), wakimchochea Bi. Pili. Wahudumu wa kike katika kasri la Bwana Maksuudi katika *Utengano* (Mohamed, 1980) wanaonyesha utumwa na utegemezi ambao ukombozi wa Maimuna unaupinga. Katika *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990), Da Rupia, anayejizalishia kipato kwa kutembeza mafuta mazuri kutoka Dubai (uk. 90), anathibitisha kwamba hata katika nafasi ya ujenzi mwanamke wa Khamis anatenda. Wanajamii walioathirika katika *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010), wanaohudumiwa na kitengo cha matatizo ya wanawake katika ghorofa ya Nana (uk. 198), wanaonyesha ukubwa wa tatizo linalohalalisha taasisi yake, nao wanawake wa kijiji katika *Kamwe si Mbali Tena* (Mohamed, 2014), wakishirikiana na Samira na Mwavile, wanaonyesha nguvu ya umoja katika kudai haki ya ardhi.


Wajenzi pia hubeba ushahidi wa dhuluma zinazoendelea, ambao bila wao hoja ya uwezeshaji ingekosa uzito wake. Katika *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990), Masika na Mwatima wanatajwa kama makahaba (uk. 67–68), naye Bi. Time anasimulia jinsi mwanamume alivyomziba kinywa na kumwekea noti ya shilingi kumi juu ya kifua akimwambia asimwambie mtu (uk. 80). Vivyo hivyo, kwenye kipindi cha “Dukuduku” katika *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010), wanawake kama Bi.Kivumbasi wanaeleza dhuluma za kulazimishwa kuolewa na kukosa uhuru wa kuchagua waume, ushuhuda unaohalalisha taasisi za Nana machoni mwa msomaji. Kimsingi, matokeo haya yanaonyesha kuwa wajenzi ni kumbukumbu hai ya tatizo, nao wakuu na wasaidizi ni jibu lake. Kwa mujibu wa Card (1988), wao ndio wanaojenga jamii ambamo mhusika mkuu anatenda.

4.3. Mgawanyo wa Kazi wa Kimaudhui

Kundi	**Mifano wakilishi (riwaya)**	**Mchango kwa maudhui ya uwezeshaji**
Wakuu	Semeni (*Asali Chungu*); Maimuna (*Utengano*); Asumini (*Tata za Asumini*); Nana (*Nyuso za Mwanamke*); Samira (*Kamwe si Mbali Tena*)	Hubeba safari yenyewe ya uwezeshaji kama mchakato: kutoka raslimali, kupitia uamuzi, hadi mafanikio au gharama ya kuyakosa.
Wasaidizi	Bi. Pili (*Asali Chungu*); Biti Kocho, Kazija, Bi. Farashuu (*Utengano*); Miriam, Mwomboje (*Tata za Asumini*); Bi. Mkubwa, Shemsa (*Nyuso za Mwanamke*); Bi. Chani, Jokha (*Kamwe si Mbali Tena*)	Hubeba utetezi na uwezeshaji wa wanawake wenzao: uamuzi wa mmoja huwa raslimali ya mwingine; huchochea ukuaji wa wakuu.
Wajenzi	Wanawake wa mikutano (*Asali Chungu*); wahudumu wa kasri (*Utengano*); Da Rupia, Masika, Mwatima, Bi. Time (*Tata za Asumini*); wanajamii walioathirika, Bi. Kivumbasi (*Nyuso za Mwanamke*); wanawake wa kijiji (*Kamwe si Mbali Tena*)	Huwakilisha sauti ya umma na hali halisi ya jamii inayohalalisha na kuunga mkono uwezeshaji; ni kumbukumbu hai ya tatizo.

Tak 2: Jedwali la Uainishaji wa wahusika wanawake na mchango wa kila kundi kwa maudhui ya uwezeshaji

Mgawanyo katika Jedwali 2 unathibitika pia kwa takwimu. Utafiti uliainisha mifano ishirini na saba ya uwezeshaji kwa aina tano, yaani kijamii (5), kielimu (5), kiuchumi (6), kisiasa (6) na kisaikolojia (5); Kielelezo cha Tak 3 kinaonyesha mifano hiyo kwa makundi ya wahusika wanaoibeba.



Tak 3: Mifano 27 ya uwezeshaji ya utafiti kwa aina na kundi la mhusika anayeibeba (Chanzo: data za utafiti)

Wahusika wakuu wanabeba mifano tisa kati ya kumi na tano ya uwezeshaji wa kijamii, kielimu na kisaikolojia, aina zinazohusu safari ya nafsi ya mhusika, ilhali wasaidizi wanabeba mifano sita kati ya kumi na miwili ya uwezeshaji wa kiuchumi na kisiasa, aina zinazohusu utetezi wa wengine; wajenzi wanajitokeza mara moja (Da Rupia), na mifano mitatu inabebwa kwa pamoja au na wahusika ambao utafiti haukuwaainisha (Samira na Mwavile; Miriam na Asumini; Biti Sururu).

Mjadala wa jumla wa uainishaji huu unaibua hoja kuu tatu. Kwanza, Khamis ametekeleza mgawanyo wa kazi wa kimaudhui: safari kamili ya raslimali hadi mafanikio inabebwa na wakuu, nguvu ya uamuzi kwa niaba ya wengine inabebwa na wasaidizi, na muktadha unaofanya yote hayo kuwa ya lazima unabebwa na wajenzi, kama Kielelezo cha Tak 3 kinavyoonyesha. Muundo huu unaeleza kwa nini maudhui ya uwezeshaji katika riwaya hizi yanahisiwa kuwa ya jamii nzima, na unalingana na ngazi tatu za Harvey (1965).

Pili, mgawanyo huu unajumuisha wahusika hasi na wanaoshindwa: Salila anaonyesha tamaa na kiburi kuhusu uuzaji wa ardhi ya mamake (Mohamed, 2014, uk. 168), Bi. Amina anawakilisha ufisadi wa tabaka la juu, na Asumini na Semeni wanashindwa na mfumo licha ya mwamko wao; kwa kuwaweka kando ya mashujaa, Khamis anaepuka usawiri wa kimahubiri. Tatu, ulinganifu kati ya nadharia ya uhusika na matini za Khamis unaonyesha kwamba uainishaji uliotumika hapa si kigezo cha nje kilicholazimishwa, bali ni muundo ambao mwandishi mwenyewe ameujenga kwa uangalifu (Mohamed, 1995); kwa mtazamo wa Phelan (1996), wahusika hawa hufanya kazi kimimetiki kama picha za wanawake halisi, kimaudhui kama wabebaji wa hoja ya uwezeshaji, na kisanii kama sehemu ya muundo wa makusudi wa mwandishi.

Kwa muhtasari, matokeo haya yanathibitisha tahadhari ya Osoro (2003) kwamba maendeleo hayajakamilika, kwani hata katika riwaya za kisasa wapo wanaoshindwa; lakini yanaonyesha pia, kinyume na taswira ya mwanamke-mhanga aliyoirekodi Bertoncini-Zúbková (1996), kwamba katika riwaya za Khamis mhanga hasimami peke yake: anazungukwa na wasaidizi wanaomtetea na jamii ya wanawake inayomtaka aende mbele.

5. Hitimisho

Kwa kuhitimisha, makala hii inaonyesha kwamba wahusika wanawake sabini na tano wa riwaya teule za Khamis si idadi tu, bali ni mfumo wa kimuundo wenye mgawanyo bayana wa kazi za kimaudhui: wakuu hubeba mchakato, wasaidizi hubeba utetezi, na wajenzi hubeba muktadha. Hata wahusika wanaoshindwa, kama Asumini, ni sehemu ya hoja ya uwezeshaji kwa kuonyesha gharama ya mfumo kandamizi. Mtunzi anawatumia wahusika hawa kama nyenzo ya kuonyesha kwamba uwezeshaji wanawake ni mchakato wa jamii nzima. Makala hii inatoa michango mitatu: wa kimbinu, kwa kuonyesha kwamba uainishaji wa nadharia ya uhusika unaweza kufungamanishwa na mihimili ya uwezeshaji ili kupima nani anayebeba uwezeshaji katika muundo wa kazi; wa kinadharia, kwa kuthibitisha kwa data za fasihi ya Kiswahili kwamba uainishaji wa Wamitila (2008) unalingana na ngazi za Harvey (1965) na kazi tatu za Phelan (1996); na wa kielimu, kwa kutoa kiunzi cha kufundishia riwaya hizi shuleni na vyuoni.

Mwisho, makala hii ni mchango muhimu katika kuendeleza utafiti kuhusu nafasi ya wanawake katika riwaya ya Kiswahili, kwa kuwa uhakiki wa wahusika wa kike umekuwa ukijikita katika taswira na matatizo yao badala ya muundo wao. Inapendekezwa kwamba uainishaji huu upimwe kwa riwaya kumi za Khamis zilizobaki; kwamba uchunguzi linganishi ufanywe kwa waandishi wengine wa Kiswahili, kama vile Euphrase Kezilahabi, Ken Walibora na Clara Momanyi, ambao nao wameshughulikia kwa mapana nafasi ya mwanamke katika riwaya zao; na kwamba tanzu nyingine za Khamis, yaani ushairi, tamthilia na hadithi fupi, zichunguzwe kwa kipimo

Marejeleo

Batliwala, S. (1994). The meaning of women's empowerment: New concepts from action. Katika G. Sen, A. Germain, & L. C. Chen (Wah.), *Population policies reconsidered: Health, empowerment, and rights* (kur. 127–138). Harvard University Press.

Bertoncini-Zúbková, E. (1996). *Vamps and victims: Women in modern Swahili literature. An anthology*. Rüdiger Köppe.

Bertoncini-Zúbková, E., Gromov, M. D., Khamis, S. A. M., & Wamitila, K. W. (2009). *Outline of Swahili literature: Prose fiction and drama* (2nd ed.). Brill.

Bogdan, R. C., & Biklen, S. K. (1992). *Qualitative research for education: An introduction to theory and methods* (2nd ed.). Allyn and Bacon.

Bryman, A. (2004). *Social research methods* (2nd ed.). Oxford University Press.

Card, O. S. (1988). *Characters and viewpoint*. Writer's Digest Books.

Chatman, S. (1978). *Story and discourse: Narrative structure in fiction and film*. Cornell University Press.

Cornwall, A. (2016). Women's empowerment: What works? *Journal of International Development, 28*(3), 342–359. https://doi.org/10.1002/jid.3210

Fakih, S. J. (2017). *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena: Utafiti linganishi* [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania]. http://repository.out.ac.tz/1573

Forster, E. M. (1927). *Aspects of the novel*. Harcourt, Brace.

Frye, N. (1957). *Anatomy of criticism: Four essays*. Princeton University Press.

Gromov, M. (2022). Depiction of the younger generation in Kenyan Swahili women's prose in the twenty first century. *The Nairobi Journal of Literature, 10*(1), 81–98. https://uonjournals.uonbi.ac.ke/ojs/index.php/literature/article/view/1246

Harvey, W. J. (1965). *Character and the novel*. Chatto & Windus.

Kabeer, N. (1999). Resources, agency, achievements: Reflections on the measurement of women's empowerment. *Development and Change, 30*(3), 435–464. https://doi.org/10.1111/1467-7660.00125

Kabeer, N. (2005). Gender equality and women's empowerment: A critical analysis of the third Millennium Development Goal. *Gender & Development, 13*(1), 13–24. https://doi.org/10.1080/13552070512331332273

Keller, B., & Mbewe, D. C. (1991). Policy and planning for the empowerment of Zambia's women farmers. *Canadian Journal of Development Studies, 12*(1), 75–88. https://doi.org/10.1080/02255189.1991.9669421

Kezilahabi, E. (1980). *Rosa Mistika*. Kenya Literature Bureau.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International.

Malhotra, A., Schuler, S. R., & Boender, C. (2002). *Measuring women's empowerment as a variable in international development*. World Bank.

Mohamed, S. A. (1977). *Asali chungu*. Shungwaya Publishers.

Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Longman Kenya.

Mohamed, S. A. (1990). *Tata za Asumini*. Longman Kenya.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili: Tamthilia, riwaya na hadithi fupi*. East African Educational Publishers.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za mwanamke*. Longhorn Publishers.

Mohamed, S. A. (2014). *Kamwe si mbali tena*. Oxford University Press.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Vide-Muwa Publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Sasa Sema Publications.

Mosedale, S. (2005). Assessing women's empowerment: Towards a conceptual framework. *Journal of International Development, 17*(2), 243–257. https://doi.org/10.1002/jid.1212

Msokile, M. (1993). *Uchambuzi na uhakiki wa riwaya: Kidato cha nne*. Dar es Salaam University Press.

Mugambi, E. K. (1983). *Kilio cha wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed* [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/155121

Muia, S. T., Mutua, J., & Makoti, V. (2023). Usawirishaji wa uhusika katika riwaya za Rosa Mistika na Maisha Kitendawili. *Research Journal in African Languages, 4*(2). https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1053

Osoro, M. G. (2003). *Uhakiki wa riwaya za Ahmed Mohamed katika misingi ya kifeministi* [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/18743

Phelan, J. (1996). *Narrative as rhetoric: Technique, audiences, ethics, ideology*. Ohio State University Press.

Rowlands, J. (1995). Empowerment examined. *Development in Practice, 5*(2), 101–107. https://doi.org/10.1080/09614529510001 57074

Rowlands, J. (1997). *Questioning empowerment: Working with women in Honduras*. Oxfam.

Rowlands, J. (1998). A word of the times, but what does it mean? Empowerment in the discourse and practice of development. Katika H. Afshar (Mh.), *Women and empowerment: Illustrations from the Third World* (kur. 11–34). Macmillan.

Ruto, M. C. (2015). *Matatizo ya mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke* [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/93693

Schuler, S. R., & Hashemi, S. M. (1994). Credit programs, women's empowerment, and contraceptive use in rural Bangladesh. *Studies in Family Planning, 25*(2), 65–76. https://doi.org/10.2307/2138085

Sen, G. (1993). Women's empowerment and human rights: The challenge to policy. Katika *Population summit of the world's scientific academies* (kur. 363–375). National Academy Press.

Shafi, A. S. (1979). *Kuli*. Tanzania Publishing House.

Suakei, S. (2013). *Usasa na mwanamke wa kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya S. A. Mohammed* [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

United Nations. (1995). *Beijing Declaration and Platform for Action*. United Nations. https://www.un.org/womenwatch/daw/beijing/platform/

Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Focus Publications.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.